


Kuhesabu wanyama



✎ Zanele Buthelezi, Thembani Dladla,
Clare Verbeek
☑ Rob Owen
📄 Matteo E. Mwita
📄 1
🗨️ Kiswahili! MS



Global Storybooks

globalstorybooks.net


Kuhesabu wanyama

✎ Zanele Buthelezi, Thembani Dladla,
Clare Verbeek
☑ Rob Owen
📄 Matteo E. Mwita




This work is licensed under a Creative Commons
[Attribution 3.0 International License](https://creativecommons.org/licenses/by/3.0).
<https://creativecommons.org/licenses/by/3.0>







Tembo mmoja anakwenda
kunywa maji.

Twiga wawili wanaenda
kunywa maji.






Nyati watatu na ndege
wanne nao wanaenda
kunywa maji.





Tembo mmoja anakunywa
maji na simba.

Swala watano na ngiri sita
wanatembea kuelekea
kwenye maji.




Simba mmoja
anaunguruma. Naye
anataka kunywa maji. Nani
anamwogopa simba?





Punda milia saba
wanakimbia kuelekea
kwenye maji.



Vyura wanane na samaki
tisa wanaogelea kwenye
maji.